

UTENZI WA MWANAKUPONA NA MFUNGAMANO WA MAFUNDISHO YA KIISLAMU

Amina Ali Khamis
Mwalimu wa Skuli ya Sekondari ya Faraja
amralikh@gmail.com
0778859703

Na
Gora Akida Haji
Mwalimu wa Skuli ya Sekondari ya Faraja
hajigora82@gmail.com
0773127095

IKISIRI

Tenzi za kale katika fasihi ya Kiswahili zimekuwa na mchango mkubwa katika kuakisi utamaduni na historia ya mswahili wa mwambao wa Afrika ya Mashariki. Utenzi wa Mwanakupona ni miongoni mwa tenzi za kale katika fasihi ya Kiswahili. Wahakiki na wataalamu wa fasihi kwa ujumla wamekuwa na mijadala mizito ndani ya kazi hii, katika kuangalia namna alivyochorwa mwanamke ndani ya utenzi huu. Kuna wanaodai kuwa, mwanamke amechorwa katika mchoro hasi na kuna wale wanaotetea na kudai kachorwa katika mchoro chanya. Makala hii imelenga moja kwa moja kuuchambua utenzi wa mwanakupona, kwa kuangali ni vipi unafungamana na dini ya kiislamu katika mafundisho yake kwa kurejelea aya za Qur-ani na hadithi za Mtume (s.a. w), katika maisha ya ndoa. Data ya utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia muongozo wa nadharia ya Uislamu kama ilivyochambuliwana Prof. Sengo. Matokeo ya utafiti huu yanathibitisha kuwa, kila alichokiandika kwa lengo la kumfunza mwanawe na jamii yake kwa ujumla, aliegemea na alizingatia mafundisho ya dini ya Kiislamu kama yalivyoamrisha katika Qur-ni na hadithi za Mtume (SAW). Utafiti umeonesha kuwa utenzi wa mwanakupona umemchora mwanamke kwa nafasi stahiki kwa kumuonesha kuwa mwanamke ni mlezi wa mume wake kwa mahaba na huba pia ni mlezi wa familia kwa ujumla. Aidha imemuonesha mwanamke ni mwalimu mwenye dhima ya kufunza jamii na kurithisha utamaduni wa jamii hiyo. Ukarimu, huruma na upendo wa mwanamke kwa mume wake, ndivyo vinavyomwandisha hadhi na heshima stahiki kwa mume wake na jamii yake kwa ujumla. Hivyo makala hii inakusudia kuchambua utenzi wa MWANAKUPONA na mfungamano wa mafundisho ya kiislamu.